# LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

Justice Lugakingira House, Kijitonyama, P. O. Box 75254, Dar Es Salaam, TANZANIA
Telephone: 2773048, 2773038, Fax: 2773037, E-mail: lhrc@humanrights.or.tz
Website www.humanrights.or.tz

## Tamko:
## Ufafanuzi wa Kisheria katika Mjadala wa Bunge la Bajeti, 2018/2019

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kinapenda kuikumbusha Serikali pamoja na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mambo kadhaa kutokana na mjadala wa Bajeti unaoendelea Bungeni katika masuala yafuatayo:-

Kutokana na mjadala unaloendelea Bungeni kuhusu Bajeti ya Maendeleo ya Serikali 2018/19, ambapo mapendekezo ya Sheria ya Fedha, 2018 aliyoletwa na Serikali katika kuhamisha asilimia 65% ya ushuru wa mauzio ya nje kutoka Mfuko wa Maendeleo ya Korosho kwenda Akaunti ya pamoja ya Hazina.

Mabadiliko hayo **yataathiri moja kwa moja haki za msingi za wakulima wa zao la korosho** katika mikoa 17 ikiwemo Mikoa ya Kusini, hususani haki ya kupata maendeleo na haki ya kufanya kazi kama ilivyoainishwa katika Ibara ya 8 (1) (a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977 inasema kwamba:

*"Wananchi ndio msingi wa mamlaka yote, na serikali itapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi kwa mujibu wa Ibara hii."*

Kutokana na mapendekezo ya mabadiliko hayo kupitia Sheria ya Fedha, 2018 , kifungu 17A cha Sheria ya Tasnia ya Korosho, 2009 kwa kufuta kipengele kidogo cha pili na kuweka kipengele cha maudhui mengine ambapo kifungu cha tatu kinaondolewa na kubaki kifungu namba 2 ambacho kinasomeka kama ifuatavyo:

*"Jumla ya makusanyo yote ya ushuru wa mazao ya nje ambayo yatakusanywa chini ya kifungu kidogo cha pili 2 yataingizwa kwenye Mfuko jumuifu"*

**Board of Directors:**
Prof. Geoffrey R.V. Mmari - Chairperson, Ms. Athanasia Soka(Adv) - Vice Chairperson,
Dr. Helen Kijo-Bisimba - Secretary, Mr. Francis Stolla (Adv) - Member, Ms. Emeline Mboya - Member,
Ms. Pili Mtambalike - Member Mr. Thaddeo W. Mashera - Member

Katika hatua nyingine Kituo kimesikitishwa na majibu ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye katika majibu yake alikana kutambua Mfuko wa Maendeleo ya Korosho na kusema kwamba mfuko huo haujaanzishwa na Sheria ya Bunge, na hivyo hata pesa za mfuko huo ni mali ya umma na sio mali ya bodi kwani kazi yake ni kukusanya fedha kwa niaba ya serikali.

Hivyo, si vema kujitikia katika mabishano kuhusu uhalali wa fedha hizo kuwa ni mali ya umma au la, kwani ni wazi kwamba fedha zote zinazokusanya na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mali ya umma na inapaswa kugawanywa kwa mujibu wa makubaliano na sheria za nchi. Mathalani ibara 135 (1) na (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 inameainisha matumizi ya fedha zitakazo kuwa kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina pamoja na matumizi ya fedha zisiokuwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina, ambazo zitatumika kwa matumizi maalumu yaliyowekwa kisheria.

Mfuko wa Maendeleo ya Korosho umetajwa na kupewa uhalali katika kifungu namba 17A cha Sheria ya Tasnia ya Korosho, 2009 kupitia Mabadiliko ya Sheria ya Fedha namba 15 ya 2010 kifungu namba 4 inayoweka mgawanyo wa ushuru wa mauzo ya nje kwa kiwango cha asilimia 65% kwenda kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Korosho. Kwa maana hiyo, Mfuko wa Maendeleo ya Korosho ni mfuko halali uliowekwa kupitia sheria hiyo.

Kwa mujibu wa kifungu cha 17A cha Sheria ya Tasnina ya Korosho, 2009 asilimia 65% ya makusanyo ya ushuru wa mauzo ya nje ya korosho inapaswa kwenda katika Mfuko wa Maendeleo ya Korosho na aslimia 35% kwenda Mfuko Mkuu wa Hazina. Kitendo cha maelezo Mwanasheria Mkuu wa Serikali kutotambua mfuko huo ni sawa na kutotambua kifungu cha 17A cha Sheria hiyo iliyotungwa na Bunge inayotambua uwepo wa Mfuko wa Maendeleo ya Korosho, hivyo maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kutouambua mfuko wa Maendeleo ya Korosho ni kulidharau Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lililopitisha sheria hiyo kupitia mabadiliko ya Sheria ya Fedha yaliyofanyika 2010.

Pia, ufafanuzi wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali uliohusisha maamuzi ya kesi namba 204 ya mwaka 1999 pamoja na maamuzi ya Mahakama ya Rufani katika kesi namba 18 ya mwaka 2001 si sehemu ya mjadala wa hoja zinazoibuliwa na kutetewa na wawakilishi wa wananchi bungeni, pamoja na wadau wa Sekta ya Kilimo, kwani maamuzi ya kesi hizo haziondoi uhalali wa kifungu cha 17A cha Sheria ya Tasnia ya Korosho ya mwaka 2009.

**Board of Directors:**
Prof. Geoffrey R.V. Mmari - Chairperson, Ms. Athanasia Soka(Adv) - Vice Chairperson,
Dr. Helen Kijo-Bisimba - Secretary, Mr. Francis Stolla (Adv) - Member, Ms. Emeline Mboya - Member,
Ms. Pili Mtambalike - Member Mr. Thaddeo W. Mashera - Member

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu **kinaishauri** Serikali kupitia Wizara ya Fedha kutokufanya mapendekezo katika Sheria ya Fedha, 2018 mpaka pale watakapopata maoni ya wananchi walio wengi hususani walengwa wa sheria hiyo.

**Imetolewa leo tarehe 26/06/2018 na,**

**Felista Mauya**

**Kaimu Mkurugenzi Mtendaji**
**Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu**

**Board of Directors:**
Prof. Geoffrey R.V. Mmari - Chairperson, Ms. Athanasia Soka(Adv) - Vice Chairperson,
Dr. Helen Kijo-Bisimba - Secretary, Mr. Francis Stolla (Adv) - Member, Ms. Emeline Mboya - Member,
Ms. Pili Mtambalike - Member Mr. Thaddeo W. Mashera - Member